**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KATIKA KUFUNGUA KIKAO KAZI CHA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI TAREHE 24 JULAI, 2020 KATIKA UKUMBI WA MORENA HOTEL JIJINI DODOMA**

**Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
**Wajumbe wa Tume,**
**Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
**Wasimamizi wa Uchaguzi,**
**Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
**Mabibi na Mabwana.**

**Habari za Asubuhi!**

Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima kwa siku ya leo, ambapo tumeweza kukutana hapa kwa ajili ya kikao kazi hiki muhimu cha Wasimamizi wa Uchaguzi ikiwa ni sehemu ya maaandalizi kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliopangwa kufanyika tarehe 28 Oktoba, 2020.

Kwa nafasi ya pekee, ninapenda kuwapongeza wote kwa kuteuliwa na Tume kuratibu na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020 katika maeneo yenu. Zoezi hili ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu, sina shaka kwamba uzoefu,

taaluma na uwezo wa kiutendaji mlionao utawawezesha kutekeleza majukumu yaliyopo mbele yenu kwa ufasini mkubwa.

**Ndugu Washiriki**

Kufuatia kukamilika kwa zoezi la uteuzi wa watendaji mkiweno ninyi Wasimamizi wa Uchaguzi, Tume imeona kwamba ni vema tukafanya kikao cha pamoja ili kupeana taarifa na kufahamishana kuhusu mambo ambayo tunapaswa kuyazingatia katika kipindi hiki tunapoelekea Uchaguzi Mkuu. Vilevile, kikao hiki ni nafasi ya kubadilishana na kupeana uzoefu wa utekelezaji wa shughuli za uchaguzi ili kuhakikisha tunaepusha dosari ambazo zinaweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

**Ndugu Wasimamizi wa Uchaguzi,**

Naomba nitumie kikao hiki kusisitiza kuwa mnalo jukumu la kuhakikisha kuwa mnafanikisha uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ambao umepangwa kufanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 katika majimbo na kata zilizopo katika maeneo yenu.

Nawasihi muandae mipango mizuri ya uendeshaji wa uchaguzi; muyaelewe vema mazingira ya maeneo yenu yanayoweza kuathiri uchaguzi katika hatua mbalimbali kama vile hali ya kijiografia, hali ya usafiri na mawasiliano; hali ya kisiasa na kijamii; hali ya kiuchumi; na

matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea na yanayoweza kuathiri ufanisi wa uchaguzi kwa ujumla.

Vilevile mnalo jukumu la kuwasimamia na watendaji wa uchaguzi waliopo chini yenu ili nao pia watekeleze majukumu yao kwa ueledi na umakini mkubwa.

**Ndugu washiriki**

Kufuatia uteuzi wenu kuwa Wasimamizi wa Uchaguzi, ninyi sasa ni sehemu ya Watendaji wa Tume. Hivyo sina budi kuwapa taarifa ya hatua zilizofikiwa hadi hivi sasa katika maandalizi ya uchaguzi mkuu.

**Fedha za Uchaguzi**

**Ndugu Washiriki,**

Kama ambavyo mmeshaona, Tume imewatumia fedha kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uchaguzi katika halmashauri zenu na maandalizi ya kutuma fedha awamu ya nyingine yanaendelea. Napenda kuwasisitiza kuzingatia Sheria za Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sheria ya Uchaguzi na Maelekezo yanayotolewa na Tume wakati wa matumizi ya fedha hizo na si vinginevyo.

**Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

**Ndugu Washiriki,**

Katika maandalizi, Tume imekamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao ulifanyika mara mbili kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Awamu ya kwanza ilianza tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020 kwa nchi nzima na awamu ya pili ya zoezi ilikuwa tarehe 17 Aprili, 2020 na kukamilika tarehe 04 Mei, 2020. Awamu ya pili ya uboreshaji ilifanyika sambamba na uwekaji wazi wa daftari la awali la awamu ya kwanza katika vituo 37,814 vilivyotumika katika zoezi la uboreshaji awamu ya kwanza. Tume iliendesha zoezi la uwekaji wazi wa Daftari la awamu ya pili kwa siku 4 kuanzia tarehe 17 - 20 Juni, 2020 na zoezi hilo lilifanyika kwa kubandika daftari katika vituo vyote vilivyotumika wakati wa uandikishaji awamu ya kwanza.

Kwa awamu zote mbili za uboreshaji, jumla ya wapiga kura wapya **7,326,552** waliandikishwa sawa na asilimia **31.63** ya wapiga kura **23,161,440** walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, Jumla ya wapiga kura **3,548,846** waliboresha taarifa zao na wapiga kura **30,487** waliondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga kura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kutoa wapiga kura ambao taarifa zao zimejirudia taarifa za awali zinaonesha kuwa Daftari lina jumla ya wapiga kura takribani million **29.**

**Marekebisho ya Sheria**

**Ndugu Washiriki**

Kwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu hakukuwa na marekebisho katika Sheria za Uchaguzi, hata hivyo, Tume imefanya maboresho ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Vile vile imekamilisha maboresho ya Maelekezo ya Uchaguzi kwa ajili ya wadau na watendaji wa Uchaguzi. Sheria na Vitabu hivyo vya maelekezo mtapatiwa wakati wa mafunzo.

Hata hivyo, mmetumiwa nakala tepe (soft copies) ambazo naomba kuwasihi muendelee kuzisoma na kuzielewa ili kurahisha utendaji wenu wa kazi.

**Maadili ya Uchaguzi**

**Ndugu Washiriki**

Tume kwa kushirikiana na Serikali na Vyama vya siasa iliandaa Maadili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambayo yalisainiwa tarehe 27 Mei, 2020. Maadili hayo yameainisha mambo yanayotakiwa kuzingatiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Serikali.

Mkiwa Wasimamizi wa Uchaguzi, mtakua ndio Wenyeviti wa Kamati za Maadili katika majimbo mnayoyasimamia. Ni vema mkayasoma na kuyaelewa maadili haya kwani yameainisha mambo ambayo

tunapaswa kuyazingatia katika kipindi chote cha kampeni nanyi mnapaswa kusimamia utekelezaji wake katika maeneo yenu.

**Ndugu Washiriki**

Kanuni za Maadili zinaeleza kuwa katika kipindi cha uteuzi wa wagombea, upigaji kura na katika hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi, watendaji wa Tume watatakiwa wakati wote kuwepo katika maeneo yao ya kazi. Ninawasisitiza kuzingatia hili kwani uzoefu unaonesha baadhi ya watendaji wa uchaguzi katika chaguzi zilizopita wamekuwa wakikiuka maadili haya hali iliyopelekea kuwepo kwa malalamiko. Vilevile msisite kuwasiliana na Tume kwa jambo lolote lile ambalo mnadhani linahitaji ufafanuzi.

**Uteuzi wa Watendaji**

**Ndugu Washiriki**

Tume imekamilisha zoezi la uteuzi wa Watendaji watakaosimamia na kuendesha shughuli za uchaguzi katika majimbo ya Jamhuri ya Muungano na kata za Tanzania Bara.

Watendaji walioteuliwa ni Waratibu wa Uchaguzi 28, Wasimamizi wa Uchaguzi 194, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo 742 na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata 7,912. Tume inatambua kuwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watafanya kazi chini ya Usimamizi wenu hivyo mnatakiwa

kuhakikisha mnawapangia majukumu watendaji hao ili kuwe na ufanisi katika zoezi la uchaguzi. Aidha, hakikisheni mnaandaa utaratibu utakawezesha watendaji hao kuyaelewa majukumu waliyopewa na kuyatekeleza kwa mujibu wa Sheria na maelekezo ya Tume.

**Ununuzi wa Vifaa vya Uchaguzi**

**Ndugu Washiriki**

Tume inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 sambamba na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo. Baadhi ya vifaa vimekamilika na vimeanza kupokelewa katika bohari ya Tume. Ni matarajio yetu kuwa vifaa vyote vitakuwa tayari mapema ili visambazwe kwa wakati katika maeneo yenu kwa ajili ya kufanikisha mchakato wa uchaguzi. Mnatakiwa kuandaa utaratibu wa kuvipokea, kuvihifadhi katika hali ya usalama na kuhakikisha vifaa hivi vinafika katika vituo vya kupigia kura kwa wakati siku ya uchaguzi.

Aidha, natoa rai kwenu kukagua na kuhakikisha vifaa mtakavyopokea viko sahihi wake na ikionekana kuna mapungufu yatolewe taarifa mapema ili Tume iyafanyie kazi kwa haraka kwani kukosekana kwa vifaa au upungufu wa vifaa kunaweza kusababisha kuharibika kwa mchakato wa uchaguzi. Kwa uchaguzi huu, Tume kwa mara ya

kwanza imewajumuisha Maafisa Ugavi katika watendaji wa uchaguzi. Hatua hii imefanyika ili kuhakikisha kwamba usimamizi na uratibu wa vifaa vya uchaguzi unafanyika vema.

## Vibali kwa watazamaji wa uchaguzi na kutoa Elimu ya mpiga kura na

**Ndugu Washiriki**

Tume imetoa vibali kwa Asasi za Kiraia 97 kwa ajilli ya kutazama Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya sheria, Tume imewasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kutoa mialiko kwa Watazamaji wa Kimataifa kwa ajili ya kutazama Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Hawa wote watafika katika maeneo yenu kwa ajili ya kutazama uchaguzi na Tume itawapa vitambulisho maalumu, niwasihi muwape ushirikiano ili waweze kutekeleza jukumu lao la utazamaji. Aidha, natoa rai kwenu kuhakikisha wanatekeleza jukumu hilo kwa kuzingatia Mwongozo wa Watazamaji uliotolewa na Tume.

**Ndugu Washiriki**

Tume imetoa vibali kwa asasi za kiraia **245** Tanzania Bara na Asasi za Kiraia **7** kutoka Tanzania Zanzibar kwa ajili ya kutoa elimu kwa wapiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Asasi hizi zitatekeleza jukumu hili la kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo yenu. Aidha, natoa rai kwenu kuhakikisha elimu wanayoitoa

inazingatia Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura uliotolewa na Tume.

## Mawakala Wa Vyama Vya Siasa Wakati Wa Uchaguzi

**Ndugu Washiriki**

Mwisho lakini si kwa kukosa umuhimu nigusie suala la Mawakala wa Vyama vya Siasa wakati wa uchaguzi. Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi na kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, Mawakala wa Vyama vya Siasa wataruhusiwa kuwepo katika vituo vya kupigia Kura. Jambo hili ni muhimu kwani linasaidia kudhihirisha uwazi katika zoezi zima. Wajibu wa Mawakala wa Vyama vya Siasa ni kuangalia kama Sheria, Kanuni, na Taratibu zilizowekwa na Tume zinazingatiwa katika mchakato mzima wa kupiga Kura hadi kutangaza matokeo. Tume katika maelekezo yake imeainisha utaratibu utakaotumika katika kuwatambulisha mawakala hawa wakati wa uchaguzi. Nawasihi kuhakikisha maelekezo ya Tume kuhusiana na utambulisho wa mawakala na utaratibu wa kuwaapisha unazingatiwa ipasavyo ili kuepusha malalamiko yanayoweza kujitokeza.

**Ndugu Washiriki**

Kwa maelezo haya machache, napenda kuwashukuru tena kwa kuitikia wito na kushiriki kikao hiki muhimu kwetu sote. Ninawatakia kikao chema na utendaji mzuri wa kazi kubwa ya Kitaifa iliyoko mbele yetu; na sasa ninapenda kutamka kwamba kikao hiki kimefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**